

Tarehe 10 Mei 2024

Mwanafunzi wa Ajabu wa Gredi ya 4 katika Austin Elementary Afuzu Shindano la Kitaifa la Tahajia

Alipokuwa akijiandaa kwa mashindano ya tahajia ya shule, wilaya na jimbo, mwanafunzi wa gredi ya nne wa Shule ya Austin Elementary Sarv Dharavane, 10, alijifunza kutahajia mamia ya maneno, kazi ngumu ambayo hatimaye ilizaa matunda. Juhudi zake zilizofanikiwa zilimshindia Shindano la 63 la Tahajia la Jumuiya ya Walimu wa Jimbo la Georgia mnamo Machi, ambalo lilijumuisha safari iliyolipiwa gharama zote hadi National Harbor, Maryland, ambapo atashindana katika shindano la kitaifa la Scripps National Spelling Bee. Mashindano ya kwanza yataanza tarehe 28 Mei. Iwapo atafaulu, atafika fainali tarehe 30 Mei.

Katika shindano la jimbo, Sarv aliwashinda wanatahajia wengine 20 kutoka gredi ya tatu hadi ya nane, wenye umri wa kuanzia miaka 10 hadi 14. Alionyesha kushangazwa na ushindi wake.

“Nilimshinda kila mtu,” alisema. “Mshindi wa pili alikuwa mwanafunzi wa gredi ya nane ambaye alishiriki katika shindano la jimbo mara nne, amewahi kushiriki katika shindano la kitaifa hapo awali, na akamaliza wa pili.”

Safari ya ushindi haikuwa rahisi. Sarv alisema alijitahidi sana kujitayarisha kwa shindano la tahajia la shule yake, akisoma kutoka kwa orodha ya maneno 450 ambayo shule ilitoa kwa washiriki. Pia alisoma maneno mengi katika kamusi ambayo hayakuwa kwenye orodha. Alitumia programu inayoitwa Word Club yenye orodha ya maneno aliyojifunza, ambayo alisema yalimsaidia sana wakati wa mashindano ya tahajia ya wilaya.

“Maneno yote yalitoka kwenye orodha ya maneno ya [Word Club],” alisema Sarv.

Alishinda ubingwa wa shindano la tahajia la 2024 la Jimbo la Georgia kwa kutahajia kwa usahihi neno “dashiki.” Wazazi wake, Shailesh Dharavane na Shilpa Tupe, walimsaidia kujiandaa kwa shindano hilo, na mama yake hata alimpeleka kwenye maktaba na kuchagua vitabu vyta kusoma.

“[Sarv] ni mwerevu, hakuna shaka kuhusu hilo,” baba yake, Shailesh Dharavane alisema. “Lakini mamake alifanya kazi kubwa ili kuhakikisha tumefika hapa.”

“Tunajivunia yeye sana,” alisema Shilpa Tupe, anayemwita mwanawewe Ensaiklopidia. “Hatukuwahi kufikiria kuwa angefuzu shindano la kitaifa katika jaribio lake la kwanza la kutahajia, lakini tulijua angejitetahidi awezavyo. Hajawahi kuzungumza juu ya kushinda shindano hilo. Kila mara alisema, ‘Nitajaribu niwezavyo katika kila ngazi,’ na tulijua atafanya hivyo.”

Wanafunzi wenzake, walimu, na usimamizi wa Austin Elementary walimsherehekeea mnamo tarehe 8 Mei, wakimtakia heri katika shindano la kitaifa.

"Tuna furaha sana kwamba anaelekea kuwakilisha shule, wilaya ya shule, na jimbo katika tahajia ya kitaifa," alisema Mwalimu mkuu wa Shule ya Austin Elementary Austin Avis Mooneyham.

Sarv amerudi kwa mambo yale yale ya msingi anapojitayarisha kwa tahajia ya kitaifa kwa kusoma upya kamusi na vitabu vingine. Pia anafanya mazoezi ya msamiatu wake akijiandaa kwa shindano hilo.

Anasema kusoma ni muhimu ili kushinda shindano la tahajia na kufanikiwa katika shughuli na mambo mengine. Sarv anawahimiza wanafunzi wengine kutafuta vitabu vinavyowavutia na kukuza upendo wa kujifunza, kuchunguza na kufurahia wanaposoma kila ukurasa.

"Soma vitabu vyako, vitabu vyote," Sarv alisema. "Ikiwa husomi vitabu, hautafika popote."

Kila la heri kwa Sarv na familia yake wanaposhiriki katika shindano la Scripps National Spelling Bee. Tutawafuatilia na kuwashangilia.

XXX